Jarida la

Nchi Yetu

Limeandaliwa na Idara ya Habari-MAELEZO JARIDA LA MTANDAONI TOLEO LA Juni-Julai 2018

Dreamliner: Ndoto Iliyotimia

- Rais Magufuli: Itaongeza Mapato, Heshima ya Nchi
- Vyombo vya Habari Kimataifa Vyaisifu Tanzania

Tabasamu la Obama Serengeti



Bodi ya Uhariri

Mwenyekiti

Dkt. Hassan Abbasi
Mkurugenzi-Idara ya Habari-MAELEZO

Wajumbe

Rodney Thadeus
Jonas Kamaleki
John Lukuwi
Elias Malima
Casmir Ndambalilo

Msanifu Jarida

Hassan Silayo

Huduma zitolewazo MAELEZO

1.Kutangaza Utekelezaji wa Serikali.
2.Kuuza Picha za Viongozi wa Taifa na Matukio Muhimu ya Serikali.
3.Kusajili Magazeti na Majarida
4.Kukodisha Ukumbi kwa Ajili ya Mikutano na Waandishi wa Habari.
5.Rejea ya Magazeti na Picha za Zamani
6.Kupokea Kero Mbalimbali za Wananchi.

Jarida hili hutolewa na:

Idara ya Habari-MAELEZO
S.L.P 25
Dodoma-Tanzania
Baruapepe:maelezo@habari.go.tz
Blogu: blog.maelezo.go.tz
Website: www.maelezo.go.tz

TAHARIRI

NI BAJETI ILIYOLENGA KUINUA MAISHA YA WANANCHI

Bajeti ya Serikali iliyowasilishwa na kupitishwa Bungeni hivi karibuni ni bajeti inayolenga kuwainua wananchi na kuboresha maisha yao.

Tumeona jinsi Wabunge wa Chama Tawala na Vyama vya Upinzani wakiiunga mkono kwa namna ilivyoondoa kero zilizokuwa zikiwasumbua wananchi hasa wa kipato cha chini.

Kwa mara ya kwanza ndani ya kipindi cha miaka takribani 57 ya uhuru, Bajeti Kuu ya Serikali haikupandisha bei za vinywaji na sigara zinazotengenezwa nchini ili kulinda viwanda vya hapa nchini. Kwa jinsi hii wananchi wa kipato cha chini wataweza kupata bidhaa hizi bila ongezeko la bei.

Kuondoa ushuru kwenye taulo za kike ni jambo ambalo Bajeti Kuu ya Serikali imelifanya na kufurahiwa na wabunge wengi hasa wanawake ambao ni wawakilishi wa wananchi. Baadhi ya wanafunzi wa kike wamekuwa wakishindwa kwenda shule wanapoingia katika hedhi kwa kukosa hela ya kununua taulo hizo kutokana na bei kuwa kubwa. Ni jambo la kupongezwa na wananchi wengi kwa ujumla.

Bajeti pia imelenga kuboresha kilimo, ikiwemo miundombinu yake kama vile ya umwagiliaji. Ikumbukwe kuwa kilimo ni shughuli ya kiuchumi inayotegemewa na watanzania wengi, hivyo kuboresha sekta hii ni kuonesha jinsi Serikali inavyowajali watu wake.

Serikali imezidi kutenga fedha kwa ajili ya miradi mikubwa ambayo itaboresha maisha ya wananchi ikiwemo ya ujenzi wa Reli ya Kisasa (Standard Gauge), barabara na madaraja.Aidha, serikali imetenga fedha kwa ajili ya mradi mkubwa wa kuzalisha umeme wa Stiegler's Gorge na pia ununuzi wa ndege ili kuboresha usafiri wa anga.

Kuboreshwa kwa usafiri wa anga kutafanikisha shughuli za utalii na hivyo kuongeza pato la Taifa ambalo litaakisi kuongeza kipato cha mtu mmoja mmoja na taifa kwa ujumla.

Uboreshwaji wa miundombinu ya usafiri na usafirishaji utawezesha mazao kufika kirahisi sokoni na kumwezesha mkulima kupata kipato.

Jarida la Nchi Yetu linaunga mkono bajeti hii ambayo imeonesha ukweli ulio wazi kuwa Serikali ya Awamu ya Tano inalenga kuwajali wananchi kwa kuhakikisha kwamba huduma zote zinaboreshwa, jambo ambalo litawafanya waifurahie na kujivunia nchi yao. Hii ni kusema kwamba Bajeti ya 2018/19 ni ya wananchi.

Dreamliner: Ndoto Iliyotimia

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. John Pombe Magufuli akiwa katika eneo la rubani alipoipokea ndege mpya na ya kisasa aina ya Boeing 787-8 Dreamliner baada ya ndege hiyo ambayo imenunuliwa na Serikali kuwasili katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere jijini Dar es Salaam.

Na. Mwandishi Wetu- MAELEZO.

Tanzania kwa mara nyingine tenaimeuthibitishiaulimwengu kuwa kuna tofauti kubwa kati ya maneno haya mawili; mageuzi na mageresho. Mwaka 2015 wakati akiomba kura kwa wananchi, Rais Dkt. John Pombe Magufuli aliahidi mageuzi.

Anatekeleza mageuzi. Sasa ameendeleza mageuzi hayo kwa kupokea ndege nyingine kubwa, mpya na ya kwanza kwa toleo la kisasa la Boeing 787-8 Dreamliner. Katika mapokezi ya ndege hiyo Rais Magufuli, viongozi mbalimbali wa Serikali pamoja na mamia ya wananchi si tu wamepokea ndege hiyo lakini wamethibitisha kile Rais anachokisema mara kwa mara: “Watanzania

Katibu Mkuu Kiongozi, Balozi John Kijazi akitia sahihi pamoja na Katibu Mkuu (Sekta ya Uchukuzi), Dkt. Leonard Chamuriho kwa ajili ya makubaliano ambayo Serikali imeikodisha Ndege yake mpya aina ya Boeing 787-8 Dreamliner kwa Shirika la Ndege la ATCL kwa ajili ya kufanyia biashara ya usafiri wa anga.

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. John Pombe Magufuli akikata utepe pamoja na Makamu wa Rais Samia Suluhu Hassan, Waziri Mkuu Kassim Majaliwa pamoja na viongozi wengine mara baada ya kuwasili kwa Ndege mpya aina ya Boeing 787-8 Dreamliner ambayo imenunuliwa na Serikali.

tukiamua, tunaweza."

Ndugu zangu sisi ni taifa kubwa na lenye rasilimali nyinyi sana hivyo ni aibu kutokuwa na ndege, tuko watu milioni 50 na ushee na tumebarikiwa kuwa na kila kitu kuanzia madini ya kila aina, wanyama pamoja na vivutio mbalimbali, haiingii akilini kutokuwa na maendeleo, na ujio wa ndege hii umedhihirisha kwamba watanzania tunaweza," alisema Rais Magufuli akionekana mwenye furaha.

Ni Zaidi ya Ndege

Tunaweza leo kujadili sana ujio wa ndege hii pia iliyobatizwa jina kuwa "ya ndoto zetu" na kujadili usasa wake na upya wake na ufahari wake. Lakini jambo kubwa na la muhimu ni umuhimu wake kwa uchumi wa nchi.

Ndio maana akizungumza katika mapokezi hayo aliyepata kuwa Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Mambo ya Ndani, Mzee Augustine Lyatonga Mrema alisisimua wengi pale aliposema kwa kukosa ndege hasa za kimataifa ni kama Tanzania ilikuwa uchi duniani.

"Leo kwa kutuletea ndege hii Mheshimiwa Rais nakupongeza sana, umetuvika nguo mbele ya uso wa kimataifa kwani jina la Tanzania nalo litasikika katika medani za kimataifa katika usafiri wa anga," alisema Mzee Mrema kauli iliyoungwa mkono na kiongozi mwingine wa upinzani John Momose Cheyo alipongeza:

"Nilipogombea Urais miaka kadhaa nyuma na kuahidi mapesa wengi hamkunielewa. Leo Magufuli anawaletea mapesa. Ndege hii ni mapesa kwa watanzania, itachangia katika uchumi na kuleta watalii wengi." Akishadidisha faida hizo Rais Magufuli katika hotuba yake alisema baada ya ndege hiyo kufanya safari za majaribio nchini mpaka Septemba mwaka huu, itaanza mara moja safari za kimataifa ikianzia na India, Thailand na China. Rais naye akasema hii ni zaidi ya ndege:

"Ndege hii itawasaidia wafanyabiashara wa ndani na nje ya nchi, italeta watalii na ni fahari yetu kimataifa. Nchi nyingi zinazopokea watalii wengi zina mashirika yao ya ndege hivyo na sisi ndege hii itatusaidia." Ni sahihi. Takwimu za njia wanazotumia watalii duniani kwenda kwenye vivutio mbalimbali zinaonesha kuwa asilimia 70 wanatumia au wanahitaji usafiri wa ndege.

Katika mapokezi hayo ya kihistoria ya ndege, Rais Magufuli aliwashukuru watanzania kwa kumuunga mkono kwa kuchapa

"Ndugu zangu sisi ni taifa kubwa na lenye rasilimali nyinyi sana hivyo ni aibu kutokuwa na ndege, tuko watu milioni 50 na ushee na tumebarikiwa kuwa na kila kitu kuanzia madini ya kila aina, wanyama pamoja na vivutio mbalimbali, haiingii akilini kutokuwa na maendeleo, na ujio wa ndege hii umedhihirisha kwamba watanzania tunaweza".

DKT. JOHN POMBE MAGUFULI
Rais wa Tanzania

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. John Pombe Magufuli akiteta jambo na Msemaji Mkuu wa Serikali Dkt. Hassan Abbasi ndani ya ndege ya Boeing Dreamliner

kazi lakini kwa kulipa kodi kwani ndege hiyo imenunuliwa kwa fedha za watanzania wenyewe.

Mabingwa wa Usafiri wa Anga Wanena

Akizungumzia ndege aina ya Dreamliner na hususani ambayo imenunuliwa na Tanzania, bingwa wa masuala ya usafiri wa anga aliyeko nchini Marekani, Mubelwa Bandio amesema Tanzania imelamba dume kwani ndege hiyo ni ya kisasa na inatumia mafuta kwa pungufu ya mpaka asilimia 20 ikitumia mfumo wa umeme na mafuta. "Inatumia zaidi umeme badala ya mafuta." Naye rubani aliyeileta ndege hiyo kutoka Seatle, Marekani hadi Dar es Salaam, Tanzania anasema tu kwa kifupi hajawahi kuona ndege ya kisasa kama hii na safari yote ya saa 17 kutoka Marekani ilikuwa maridhawa kabisa.

Akizungumzia uendeshaji wake, Mtendaji Mkuu wa ATCL, Mhandisi mwenye shahada ya umahiri katika usimamizi wa biashara, Ladislaus Matindi ambaye pia ni bingwa wa usafiri wa anga aliyepata kuwa Mkurugenzi Katika Mpango wa Afrika na Jumuiya ya Ulaya wa Kusimamia Usafiri wa Anga, Dakar, Senegali, anasema wamejipanga na wana mikakati mitatu:

"Ndege hii watu wasidhani tumekurupuka tu kuileta, tulikuwa na mkakati wa manunuzi uliohusu tununue ndege gani na kwa nini.

Tukaweka mkakati wa maboresho ya kiutendaji na tunao mkakati wa kibiashara ambao ulianza kutekelezwa na sasa tunauhusika zaidi." Mhandisi Matindi ambaye pia ni mhitimu wa masuala ya usimamizi wa Biashara (MBA) kutoka Chuo Kikuu cha Birmingham, Uingereza, anasema katika ushindani wa kibiashara wamejipanga vyema kwa sababu wanaijua vyema sekta husika na amewataka watanzania wasitiwe wasiwasi na "manabii wa uongo."

Dunia Yaizungumzia Tanzania

Mageuzi yanayoendelea katika sekta ya usafiri wa anga nchini yamevigusa vyombo mbalimbali vya kimataifa. Shirika kubwa la Habari la China Global Television Network (CGTN) lilieleza kuwa Rais Magufuli amedhamiria kufanya mambo makubwa na anajiandaa kuleta Dreamliner nyingine. Nalo Shirika kongwe la Habari la China, Xinhua, liliieleza habari hiyo kwa anuani isemayo:

"Tanzania receives first Boeing 787-8 Dreamliner to strengthen national airline." Mtandao mashuhuri duniani kwa taarifa za usafiri na teknolojia ya anga www.intelligent-aerospace.com ulieleza ujio wa ndege hiyo kwa kuhitimisha kuwa ndege hiyo itaanzia safari za ndani na kisha za nje:

"The Intelligent Aerospace Take: The plane will eventually service an intercontinental route to Mumbai, but first, Air Tanzania is putting its new aircraft through its paces with domestic flights to Dar es Salaam and Moshi."

Mtandao wa Aviation Tribune

nao haukusita kuizungumzia ndege hiyo ya Tanzania. Taarifa ya mtandao huo wa kimataifa iko hapa:http://aviationtribune.com/airlines/africa/air-tanzania-takes-delivery-of-its-first-boeing-787-dreamliner/.

Dreamliner pia ililigusa Shirika la Utangazaji la Uingereza (BBC) ambapo habari yake moja ilizingumzia mambo matano makuu aliyoyasema Rais Magufuli katika mapokezi hayo: https://www.bbc.com/swahili/habari-44762097 Shirika la kimataifa la habari za uchumi na biashara la Bloomberg nalo lilianza kuizungumzia ndege hiyo na kuonesha matumaini kwa Tanzania kuimarika kibiashara hata kabla haijafika Dar es Salaam:

Ndege nyingine kubwa aina ya Boeing Dreamliner ya abiria 262 itawasili nchini Januari, 2020 wakati Novemba mwaka huu ndege nyingine mbili aina ya C Series Bombardier zenye uwezo wa kuchukua abiria 132 zitawasili nchini kuendeleza mageuzi katika sekta za usafiri wa anga, biashara na utalii.



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. John Pombe Magufuli akikagua ndege mpya na ya kisasa aina ya Boeing 787-8 Dreamliner ambayo imenunuliwa na Serikali mara baada ya kuwasili katika uwanja wa ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere jijini Dar es Salaam hivi karibuni.

Tabasamu la Obama Serengeti

Rais Mstaafu wa Marekani, Barack Obama akilakiwa na Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Balozi Augustino Mahiga alipowasili Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro (KIA) akitokea Hifadhi ya Taifa ya Serengeti alikotalii kwa muda wa siku nane.

Na. Mwandishi Wetu- MAELEZO.

Wakati Watanzania wakifurahia kutimia kwa ndoto ya ujio wa Dreamliner siku chache zilizopita Rais Mstaafu wa Marekani, Baraka Obama akiwa na familia yake naye alitimiza ndoto yake ya miaka mingi.

Katika kitabu chake "***Dreams From My Father***" Obama alieleza jinsi akiwa angani kwenda katika ardhi ya baba yake miaka ya 1980 alivyopita juu ya ardhi nzuri yenye nyasi na wanyama wazuri ya Serengeti ambako pia alikwenda baadhi ya maeneo na kutamani kufika mbali zaidi. Hatimaye Obama ametimiza ndoto yake kwa kufurahia maisha Serengeti kwa siku 8 alizokaa Tanzania.

Rais Mstaafu wa Marekani, Barack Obama na Mkewe Michele Obama wakiwa ndani ya Hifadhi ya Taifa ya Serengeti

Rais Mstaafu wa Marekani, Barack Obama akipokea zawadi Maalum kutoka kwa Balozi Augustino Mahiga alipowasili Uwanja wa Kimataifa wa Kilimanjaro (KIA) akitokea Hifadhi ya Taifa ya Serengeti alikotalii kwa muda wa siku nane.

Rais Mstaafu wa Marekani, Barack Obama akisalimiana na Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro Mhe. Anna Maghwira alipowasili Uwanja wa Ndege wa KIA akitokea Hifadhi ya Taifa ya Serengeti

Rais Mstaafu wa Marekani, Barack Obama akisalimiana na Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kilimanjaro ACP Hamisi Issa alipowasili Uwanja wa Ndege KIA akitokea Hifadhi ya Taifa ya Serengeti.

Mnangagwa Afanya Ziara ya Kihistoria

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. John Pombe Magufuli akiwa amesimama pamoja na mgeni wake Rais wa Zimbabwe Mhe. Emmerson Mnangagwa wakati nyimbo za mataifa mawili ya Tanzania na Zimbabwe zikipigwa katika uwanja wa ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere mara baada ya Rais huyo kuwasili nchini.

Na. Mwandishi Wetu- MAELEZO.

Ziara ya Rais wa Zimbabwe, Emerson Mnangagwa aliyoifanya hivi karibuni nchini Tanzania kwa mwaliko wa Rais Dkt. John Pombe Magufuli, inatarajia kufungua milango ya uwekezaji na kukuza biashara baina ya nchi hizo.

Akiongea baada ya kufanya mazungumzo na Rais Mnangagwa Ikulu jijini Dar es Salaam, Rais Magufuli ameeleza kwamba wamekubaliana kuimarisha zaidi uchumi wa nchi zao tofauti na uhusiano wa zamani baina ya nchi hizo ambao ulikuwa wa kisiasa zaidi.

"Mwaka 2016 biashara kati ya Tanzania na Zimbabwe ilikuwa ni shiingi bilioni 18.3, sawa na

Rais wa Zimbabwe, Emmerson Mnangagwa akikagua gwaride la heshima mara baada ya kuwasili katika uwanja wa ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere

dola za Marekani milioni 8.5, mwaka 2017 biashara ilikua na kufikia shilingi bilioni 21.1 sawa na dola za Marekani milioni 9.5. Kwa sasa kuna miradi 25 ya Zimbabwe nchini yenye thamani ya dola za Marekani milioni 32.02," alifafanua Rais Magufuli wakati akielezea umuhimu wa kuendeleza biashara kati ya nchi hizo mbili.

Katika mazungumzo hayo, Rais Magufuli ameeleza kuwa wamekubaliana kupitia Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC) kukuza biashara ambapo kuna mikataba ya ulegezaji masharti ya kibiashara katika Jumuiya hiyo ili kuwezesha biashara kufanyika kwa urahisi.

Katika kuimarisha biashara na kukuza uwekezaji nchini, Rais Magufuli amemhakikishia Rais Mnangagwa kuwa Tanzania kuna hekta milioni 44 za ardhi inayofaa kwa kilimo na hekta milioni 29 zinafaa kwa kilimo cha umwagiliaji pamoja na fursa nyingi za uwekezaji katika sekta ya kilimo, mifugo na uvuvi.

Kwa upande wake, Rais Mnangagwa alisema watanzania na wazimbabwe ni kama ndugu na kwamba Tanzania imekuwa mstari wa mbele katika kuunga mkono jitihada za ukombozi wa bara la Afrika, hivyo uhusiano huo hauna budi kuendelezwa.

Aidha, katika siku yake ya pili ya Ziara hapa nchini Rais huyo alikitembelea Chuo cha Wazazi Kaole kilichopo mjini Bagamoyo na kukikabidhi dola za kimarekani elfu 10 ikiwa ni mchango wake kwa chuo hicho ambacho aliwahi kupatiwa mafunzo ya ufundi wakati wa harakati za ukombozi wa nchi za kusini mwa Afrika. Akizungumza akiwa Chuoni hapo, Rais Mnangagwa alisema

Rais wa Zimbabwe, Emmerson Mnangagwa akiangalia moja ya sufuria waliyokuwa wakiitumia katika matumizi yao ya kila siku wakati wakisoma katika Shule ya Mafunzo ya Ufundi na Jeshi ya wapigania Uhuru ya Chama cha FRELIMO.

kuwa amefurahia kuona chuo hicho kikiendelea ambapo mwaka 1963 walitumia chuo hicho kama kambi ya kijeshi katika harakati za kupigania uhuru wa nchi za Kusini mwa Afrika ikiwemo Zimbabwe.

"Naishukuru Serikali ya Tanzania na Msumbiji kwa kuendelea kutunza sehemu hii. Pia na mimi ninapenda kuchangia kiasi cha fedha dola elfu 10 za Kimarekani,"

alieleza Rais Mnangagwa. Rais Mnagangwa alisema kuwa amefurahi kufika chuoni hapo tena, ikiwa ni miaka 58 tangu amalize masomo katika chuo hicho ambacho kilikuwa kambi ya kijeshi kikiwa na wakufunzi 58 kutoka nchi za Zimbabwe, Afrika kusini na Msumbiji.

Aidha, alisema amefarijika kuona kambi hiyo waliokuwa wakitumia wakati wa harakati za ukombozi wa nchi za kusini mwa Afrika sasa kuwa ni Chuo cha Mifugo na Kilimo. Chuo cha Wazazi Kaole, kilichoanzishwa mwaka 1963 kilitumika kutoa mafunzo ya ufundi kwa wapigania uhuru wakati wa ukombozi wa nchi za kusini mwa Afrika, ambapo baadaye kilikabidhiwa kwa chama cha TANU kabla ya kuwa Chama cha Mapinduzi. Rais Emmerson Mnangangwa aliwasili nchini Juni 28 kwa ziara ya siku mbili ambapo alikubaliana na mwenyeji wake Rais Magufuli kuendeleza ushirikiano wa kihistoria uliopo baina ya Tanzania na Zimbabwe.

Makamu wa Rais Awataka Viongozi Dar Kulinda Kuta za Bahari

Muonekano wa sehemu ya ukuta wa bahari wenye urefu wa Mita 920 uliojengwa pembezoni mwa barabara ya Barack Obama uliozinduliwa hivi karibuni na Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan.

Na. Mwandishi Wetu- MAELEZO.

Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan ameutaka Uongozi wa Jiji la Dar es Salaam kuweka mikakati madhubuti ya kulinda na kuhifadhi miundombinu ya ukuta wa fukwe za bahari ili kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabia nchi ikiwemo kusogea kwa bahari na milipuko ya magonjwa ya wanyama na binadamu.

Akizungumza katika uzinduzi wa ukuta wa fukwe ya bahari eneo la Coco Beach Jijini Dar es Salaaam, Mhe. Samia alisema ukuta huo ni miongoni mwa mipango na mikakati ya muda mrefu iliyobuniwa na Serikali kwa kushirikiana na Wadau wa Maendeleo ili kukabiliana athari za mabadiliko ya tabia nchi na hivyo kuleta tishio katika maendeleo ya kijamii na kiuchumi kwa wananchi.

"Ujenzi wa ukuta huu ni njia mojawapo ya kujihami na kupunguza athari za mabadiliko ya tabia nchi, tukiutunza vizuri ukuta huu utaweza kuishi kwa miaka zaidi ya 70, tukitunza miundombinu yake tutaweza kufurahia mandhari ya maliasili ya bahari" alisema Makamu wa Rais.

Aliitaka Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam kuimarisha miundombinu ya ukuta huo, kujenga vibaraza na kupanda bustani ya majani katika kingo za barabara za ukuta wa ufukwe huo na kufanya kuwa chanzo cha mapato cha Jiji hilo.

Aidha Mhe. Samia alisema Serikali itaendelea kushirikiana na wadau mbalimbali wa mazingira ikiwemo Mfuko wa Dunia wa kuhimili mabadiliko ya tabia nchi na kuongeza kuwa Serikali ya Awamu ya Tano itaendelea kusimamia utekelezaji wa miradi inayoendelea ya ujenzi ya ukuta wa fukwe za bahari katika maeneo mbalimbali nchini.

Kwa upande wake, Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Mhe. January Makamba alisema

Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan akizindua ukuta uliojengwa kwenye kingo za Bahari ya Hindi pembezoni mwa barabara ya Barack Obama, kulia ni Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira Mhe. January Makamba na Mwenyekiti Mkazi wa Kampuni ya Shell Bw. Axel Knospe.

mbali na ujenzi wa ukuta huo katika eneo la Coco Beach,

Serikali pia inatekeleza miradi ya ujenzi wa kuta hizo katika eneo la Kigamboni Jijini Dar es Salaam, Pangani Mkoani Tanga, Kilimani Zanzibar na Kisiwa Panza, Pemba. Aliongeza kuwa utekelezaji wa mradi huo ni sehemu ya manufaa ya ushiriki wa Tanzania katika mahusiano ya kimataifa hususani nafasi ya uanachama wa mkataba wa kimataifa wa mabadiliko ya tabia nchi na hivyo kunufaika na mifuko mbalimbali iliyosaidia udhibiti wa athari za mabadiliko ya tabia nchi katika nchi zinazoendelea.

Akifafanua zaidi, Waziri Makamba alisema mabadiliko ya tabia nchi yameleta athari kubwa katika sekta za uzalishaji mali ikiwemo kilimo, ufugaji, uvuvi na nishati hivyo Serikali itaendelea kutafuta rasilimali fedha katika mifuko ya mazingira ya dunia ili kukabiliana na athari hizo kwa ustawi wa vizazi vijavyo.

Naye Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Mhandisi Joseph Malongo alisema ujenzi wa ukuta huo ulianza mwaka 2012 kupitia mkataba wa Umoja wa Mataifa wa kudhibiti mabadiliko ya tabia nchi kwa kushirikiana na Halmashauri za Manispaa ya Ilala, Kinondoni, Temeke na Chuo Cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere (MNMA).

Mhandisi Malongo alisema ukuta huo una urefu wa mita 920, ambapo jumla ya Dola ya Kimarekani milioni 5.08 zimetumika katika utelekezaji wa miradi yote minne ya Kilimani, Kigamboni, Barack Obama na Pangani.

> ***"Serikali ya Awamu ya Tano itaendelea kusimamia utekelezaji wa miradi inayoendelea ya ujenzi ya ukuta wa fukwe za bahari katika maeneo mbalimbali nchini.***
>
> **Mhe. Samia Suluhu Hassan**

Waziri Mkuu, Mhe. Kassim Majaliwa, akiongoza zoezi la upimaji wa VVU wakati wa uzinduzi wa kampeni ya kuhamasisha upimaji wa VVU hususani kwa wanaume na kuanza ARV mapema unapogundulika kuwa na maambukizi, uwanja wa Jamhuri jijini Dodoma, kauli mbiu: Mwanaume jali Afya yako Pima VVU. (Picha na Ofisi ya Waziri Mkuu)

Waziri Mkuu Ahimiza Upimaji VVU, Kuanza Mapema Dawa Kupunguza Makali

Na. Georgina Misama- MAELEZO

Serikali imewasisitiza Watanzania hasa wanaume kupima maambukizi ya Virusi Vya Ukimwi (VVU) na kuanza mapema kutumia dawa za kupunguza makali kwa wale wataokutwa na maambukizi.

Akizindua kampeni ya kuhamasisha Watanzania hasa wanaume kupima na kuanza kutumia mapema dawa za kupunguza makali ya VVU, iliyofanyika jijini Dodoma hivi karibuni, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Kassim Majaliwa alisema lengo la kampeni hiyo ni kuwasaidia watu wanaoishi na VVU kuishi maisha bora na marefu.

Mhe. Majaliwa amesema, Serikali imeamua kuanzisha kampeni hiyo ili kutekeleza malengo ya 90 Tatu katika mapambano dhidi ya ugonjwa wa UKIMWI ifikapo mwaka 2020. Malengo hayo ya 90 tatu yanalenga kufikisha asilimia 90 ya watanzania watakaofahamu hali zao za maambukizi, asilimia 90 ya waliopimwa VVU na kugundulika waanze kutumia dawa kupunguza makali ya VVU mara moja tofauti na ilivyokuwa awali ambapo ilitegemea na kiwango cha CD4 za muathirika, na asilimia 90 ya wanaotumia dawa wawe wamepunguza makali ya VVU.

"Kwa vile tunazindua kampeni ya kupima na kuanza matumizi ya dawa za kupunguza makali ya VVU mara moja, yaani Test and Treat, natoa rai kwa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa kushirikiana na OR-TAMISEMI, kuhakikisha vitendanishi na dawa za kupunguza makali ya VVU zinapatikana katika kila kituo kitakachotoa huduma katika kila Mkoa na Wilaya," alieleza Mheshimiwa Majaliwa.

Alifafanua kuwa, kampeni hiyo inayojulikana kwa jina la 'Furaha Yangu', yenye kauli mbiu inayosema Pima, Jitambue, Ishi kwa furaha,

Waziri Mkuu, Mhe. Kassim Majaliwa, akipokea tuzo ya heshima kutoka kwa Waziri wa Nchi OR TAMISEMI Mhe. Suleiman Jaffo (kushoto) Waziri wa Nchi OWM Mhe. Jenista Mhagama (wa pili kushoto) na Waziri wa Afya Mhe. Ummy Mwalimu (kulia) ishara ya kuwa kinara wa kuhamasisha wanaume kupima VVU na kuanza ARV iwapo wanapogundulika kuwa na maambukizi ya virusi vya UKIMWI.

itadumu kwa kipindi cha miezi sita na Serikali imeridhia utaratibu huo kwa kuwa una manufaa kwa mtumiaji wa dawa na jamii kwa ujumla. "Naahidi nitakuwa balozi wa kampeni hii kwa kuhamasisha wananchi katika ziara zangu zote kupima na kuanza dawa mapema. Nitakuwa na kaulimbiu ya "Mwanaume jali afya yako, pima VVU" na ninaomba viongozi wenzangu na wanasiasa mniunge mkono" Mheshimiwa Waziri Mkuu alisisitiza.

Aidha, Mhe. Waziri Mkuu aliwahimiza wanacnhi kuanza kutumia dawa watakazopewa mara tu wanapogundulika kuwa na maambukizi ya VVU bila hata kusubiri CD4 kushuka sana. Kwa mujibu wa takwimu za utafiti uliofanyika 2016/17 zinaonyesha kuwa nchini Tanzania ni asilimia 52.2 tu ya wanaoishi na VVU wenye umri wa miaka 15 hadi 64 walitoa taarifa kuwa wanajua hali zao za maambukizi ya VVU ambapo wanawake ni asilimia 55.9 na wanaume ni asilimia 45.3 na kwamba kkiwango cha hamasa kwa wanaume kutembelea huduma za upimaji wa VVU zipo chini ukilinganisha na wanawake.

Kwa upande wake Waziri wa Afya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto Mhe. Ummy Mwalimu, alisema kuwa kati ya shilingi bilioni 269 zilizotengwa kwa mwaka wa fedha 2017/18, wizara yake imetenga bilioni 5.3 kwa ajili ya kununulia dawa za magonjwa nyemelezi kwa watu wanaoishi na VVU.

Katika kuhakikisha kampeni ya "Furaha Yangu" inafanikiwa, Serikali imeongeza vituo vya kupima VVU na kutoa ushauri nasaha kutoka vituo 5,700 mwaka 2015 hadi kufikia vituo 6,005 Machi 2018. Aidha, vituo 4365 vinatoa huduma ya kuzuia maambukizi kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto.

"Mwaka 2011 maambukizi ya VVU kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto yalikuwa juu, kiasi cha asilimia 12 ya watoto nchini walikuwa wakizaliwa na VVU. Hivi sasa maambukizi hayo yameshuka hadi kufikia asilimia 4.9. Hata hivyo Serikali imedhamiria kuhakikisha kuwa hakuna mtoto anayezaliwa akiwa na VVU", alisema Waziri Ummy.

Mwezi Oktoba mwaka 2016, Serikali ya Tanzania iliridhia wananchi wake kupima na kuanza kutumia dawa za kupunguza makali ya Virusi Vya Ukimwi kwa wale waliokutwa na maambukizi. Dawa hizo zimeonesha mafanikio makubwa, na hivi sasa Serikali imetangaza kuwa ifikapo mwaka 2019 Serikali itaanza kutoa dawa mpya za kupunguza nguvu za VVU zenye ufanisi mkubwa.

Kwa mujibu wa Wataalamu wa afya, kutumia dawa za kupunguza makali ya VVU kwa usahihi, kunapunguza haraka nguvu za VVU na pia kadri mtu anavyotumia dawa hizo ndivyo anavyopunguza uwezekano wa kuambukiza watu wengine kwa asilimia 70".

"Mwanaume jali afya yako, pima VVU na naomba viongozi wenzangu na wanasiasa mniunge mkono"
Mhe. Kassim Majaliwa

Ni Bajeti ya Kuipeleka Tanzania katika Uchumi wa Kati

Ndege mpya aina ya Boeng 787-8 Dreamliner ambayo imenunuliwa na Serikali ikitua katika Ardhi ya Tanzania wakati ikitokea nchini Marekani.

Na. Mwandishi Wetu- MAELEZO

Mwezi Juni Mwaka huu Tanzania imeshuhudia kuwasilishwa Bungeni kwa Bajeti ya mwaka 2018/2019 ambapo Serikali inatarajia kukusanya na kutumia TSh trilioni 32 ikiwa ni ongezeko la TSh Bilioni 800 ikilinganishwa na bajeti iliyopiota ambayo ilikuwa ya TSh trilioni 31.7.

Katika kutekeleza bajeti hiyo ya serikali msukumo mkubwa umeelekezwa katika ujenzi wa miundombinu pamoja na utekelezaji wa miradi mikubwa ya maendeleo ikiwemo Ujenzi wa kipande cha Reli ya Kati kwa gharama ya fedha za kitanzania Shilingi 1.4 trilioni.

Mbele ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Waziri Fedha na Mipango Dkt. Philip Mpango alisema makadirio hayo yamezingatia upatikanaji wa mapato ya Serikali kutoka katika vyanzo mbalimbali.

"Serikali katika mpango wa 2018/19 imepanga kutumia TSh trilioni 20.4 kwa matumizi ya kawaida sawa na asilimia 63 na kwamba kiasi hicho kitajumuisha TSh Trilioni 10 zitakazotumika kulipa deni la Taifa, wakati TSh trilioni 7.3 zikiwa ni mishahara ya watumishi na TSh trilioni 3 ni kwa matumizi mengineyo," alisema Dkt. Mpango.

Waziri wa fedha na Mipango alisema kuwa TSh trilioni 12 ambazo ni asilimia 37 zimetengwa kutumika kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo na katika kiasi hicho, TSh trilioni 9.8 sawa na asilimia 82.3 zitatokana na vyanzo vya mapato ya ndani na TSh trilioni 2.1 sawa na asilimia 12.7 kutoka vyanzo vya nje.

Aidha kuhusu mikopo kwenye mwaka huu wa fedha, Serikali inatarajia kukopa TSh Trilioni 5.7 kutoka katika soko la ndani. Kati ya fedha hizo, Sh4.6 trilioni zitatumika kulipa hati fungani na dhamana za Serikali zinazoiva. Alisema TSh trilioni 1.1 zinazozidi ndio mikopo mipya ambayo ni sawa na asilimia 0.9 ya Pato la Taifa."Kuongeza kasi ya utekelezaji wa miradi, Serikali inatarajia kukopa TSh3.1 kutoka soko la nje.

Akielezea miradi itakayotekelezwa Waziri Mpango alisema Sh trilioni 1.4 zitatumika kuimarisha reli ya kati na fedha zote zitapatikana kutoka kwenye vyanzo vya ndani. Pia Shirika la Ndege Tanzania (ATCL)

Waziri wa Fedha na Mipango, Mhe. Dkt. Philip Mpango akionesha begi lenye hotuba ya Bajeti ya Serikali ya mwaka wa fedha 2018/2019 bungeni Dodoma hivi karibuni.

limetengewa TSh bilioni 495 kukamilisha ununuzi wa ndege ya pili aina ya Boeing 787 Dreamliner na Bombardier Q400-8.

Kwa upande wa mradi wa kufua umeme wa maji katika Bonde la Mto Rufiji alisema TSh Bilioni 700 zimetengwa ikiwa ni kwa ajili ya ujenzi wa ofisi, bwawa na njia za kupitisha maji.

Aidha mradi mwingine wa kimkakati ni mradi wa makaa ya mawe wa Mchuchuma uliotengewa TSh bilioni 5 ili kufanikisha uzalishaji wa umeme wa 220KV, pamoja na kiasi cha Sh5 bilioni ka ajili ya maandalizi ya ujenzi wa kiwanda cha chuma cha Liganga.

Kiwanda cha General Tyre Arusha kimetengewa TSh bilioni 500 kwaajili ya kuandaa upembuzi yakinifu, ununuzi wa mitambo na mashine na kulitangaza eneo hilo kwa ajili ya kupata wawekezaji pamoja na kulipa tozo ya ardhi.

Kwa mujibu wa Waziri Mpango mradi wa magadi soda katika Bonde la Engaruka umetengewa TSh bilioni 10 kwa ajili ya kuratibu na kulipa fidia kwa wananchi watakaopisha eneo hilo, kufanya utafiti wa faida za kiuchumi, kusimamia ujenzi wa miundombimu wezeshi, kulipa tozo ya ardhi pamoja na kulitangaza kama eneo la uwekezaji. Kiasi cha Sh10 bilioni zimetengwa kwa ajili ya bidhaa za ngozi huko Zuzu, mkoani Dodoma na TSh bilioni 2 ni kwa ajili ya kuimarisha Shirika la Viwango Tanzania (TBS), katika kusimamia ubora wa bidhaa hapa nchini.

Katika hotuba hiyo Waziri mpango aliwatoa hofu watanzania kwa kuwahakikishia kuwa nchi ina akiba ya kutosha ya fedha za kigeni ambapo hadi Desemba mwaka 2017 akiba ya fedha za kigeni ilikuwa Dola za kimarekani bilioni 5.9 ikilinganishwa na Dola za kimarekani bilioni 4.3 katika kipindi kama hicho mwaka 2016.

" Mheshimiwa Spika Kiasi cha akiba ya fedha za kigeni kilichofikia Desemba mwaka 2017 kilikuwa kinatosha kugharamia ununuzi wa bidhaa kwa kipindi cha miezi sita hivyo kuzidi kiwango cha angalau miezi 4.5 kilichowekwa kukidhi matakwa ya hatua za utangamano wa umoja wa fedha kwa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki," alisema Dkt Mpango.

Kwa mwelekeo wa bajeti hii ni dhahiri Tanzania itaendelea kukua kiuchumi kama nchi na kwa mwananchi mmoja mmoja kwa kuwa miradi mingi mikubwa itaajiri watanzania wengi na kutoa fursa za kibiashara kwa wananchi wa maeneo ambayo miradi hiyo inatekelezwa.

Waziri wa Fedha na Mipango, Mhe. Dkt. Philip Mpango akiwasilisha hotuba ya Bajeti ya Serikali ya mwaka wa fedha 2018/2019 bungeni Dodoma hivi karibuni.

UFUFUAJI WA VIWANDA VYA KOROSHO WAIPAISHA MTWARA

•Asilimia 95 ya waajiriwa ni wanawake.

Na: Judith Mhina - MAELEZO

Jitihada za Serikali ya Awamu ya Tano inayoongozwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, zimezaa matunda na kuwanufaisha wananchi wa Mkoa wa Mtwara.

Hayo yamebainika Mkoani humo, baada ya Idara ya Habari-MAELEZO kupata fursa ya kutembelea viwanda viwili vilivyofufuliwa vya Micronix System LTD kilichopo Manispaa ya Mtwara Mikindani na kingine Wilaya ya Newala.

Akiongea na Mwandishi Wetu, Katibu Tawala wa Mkoa wa Mtwara, Bw. Alfred Luanda amesema Mkoa wa Mtwara umebahatika kuwa na viwanda vikubwa ambavyo vimeleta neema kwa wakazi wa eneo hilo, na kuondoa matatizo mbalimbali ambayo yalikuwa yanawakabili wananchi wa mikoa ya kusini kwa miaka mingi.

Akielezea ufufuaji wa viwanda vya kubangua korosho katika Mkoa wa Mtwara amesema "Mkoa una kila sababu ya kuishukuru Serikali kwa mipango mizuri ya ufufuaji wa viwanda vya kubangua korosho. Kwa sasa wakina mama wengi wamepata ajira za uhakika. Pia viwanda hivi vimekuwa mfano kwa wale waliovinunua na kuacha kubangua korosho wakidai biashara sio nzuri na kutoa visingizio, hii imethibitisha Tanzania ya viwanda inawezekana".

Nakuhakikishia tangu Serikali ya Awamu ya Tano ilipovalia njuga suala la kufuatilia viwanda hivyo vilivyobinafsishwa na kuhoji wahusika kutozalisha kama ilivyokusudiwa imesaidia kwa kiasi kubwa kufufua viwanda vilivyodorora.

Pia jitihada za Serikali kutafuta wawekezaji ambao wako makini na ubanguaji wa korosho umepelekea mji wa Mtwara na wakazi wa wilaya zake kupata ajira kwa asilimia kubwa hususan wakinamama ambao ni asilimia 95 wameajiriwa kwenye viwanda hivyo.

Baadhi ya wafanyakazi katika kiwanda cha Micronics System Limited wakiweka bidhaa ya Korosho iliyobanguliwa kwenye vifungashio kwa ajili ya kusafirishwa nje ya nchi kwa matumizi

Akiongea na muwekezaji wa kiwanda cha kubangua korosho cha Micronics System LTD kilichopo Newala Bw. Sunil Kawath amesema "Kiwanda kilianza kubangua gunia tisa zenye uzito wa kilo 100, kila siku, lakini kwa sasa tunabangua gunia 150 hadi 160.

Aidha, korosho ya Tanzania ni bora zaidi duniani na huzalishwa kipindi ambacho nchi nyingine hazizalishi hivyo soko lake ni bora na la uhakika" Kawath amesema anafurahishwa na ulimaji wa korosho katika maeneo ya Mtwara Mji, Newala, Masasi na Tunduru ambapo uzalishaji umeongezeka mara dufu. Wakati kiwanda kimeanza kufanya kazi uzalishaji ulikuwa mdogo, lakini mwaka hadi mwaka uzalishaji unaongezeka. Nina uhakika wakulima wanapata elimu bora ya ukulima wa korosho kutoka kwa wataalam wetu na pia pembejeo za kilimo zinapatikana zinapohitajika. Akitoa ushauri kwa Tanzania kuhusiana na zao la korosho Kawath amesema kuwa, ili Tanzania iendeelee kuwa kinara katika korosho inapaswa kuendelea kuongeza viwanda vya kubangua korosho hapa nchini badala ya kuuza korosho ghafi kwani inaweza kuzifanya nchi wanazoziuzia kupanda miti ya korosho na baadaye kuacha kununua kutoka Tanzania.

Akielezea faida za korosho na masoko aliyonayo, Kawath amesema masoko mengi kwa sasa ni nchini India, Vietnam, Falme za kiarabu, Marekani na Kenya.

Aidha, korosho hutumika kutengeneza chocolate, vinywaji mbalimbali vya baridi, pia hutumika kutengeneza keki, biskuti na vitafunwa vya aina mbalimbali ambavyo hupendwa sana duniani.

Kawath alimalizia kwa kusema Kiwanda cha Micronix System LTD, kimeajiri zaidi ya wafanyakazi 1200 ambao wanajumuisha viwanda vya Mtwara Mikindani, Newala

na Tunduru ambavyo vyote ni vya muwekezaji kutoka nchini India.

Naye mkulima wa korosho katika kijiji cha Kitangiri Mjengo, katika Wilaya ya Newala, Bw Rashid Musa amesema binafsi anamiliki miti 4200 ya korosho ambayo kwa misimu miwili iliyopita aliweza kuvuna zaidi ya tani 104 ambazo zimempatia takribani Shilingi milioni 300 .

"Korosho kwangu ndio kila kitu maana nimefanikiwa kujenga nyumba za wageni sita zenye hadhi, makazi yangu mwenyewe nyumba tatu tofauti na kuwapeleka watoto wangu shule ya Tusiime Jijini Dar-es-salaam na magari kadhaa ya kazi na ya starehe". alieleza Mussa.

Hata hivyo anaeleza kuwa anaona ana deni kubwa kwa watanzania kwa kuwa nia na madhumuni yake ni kuwa mkulima wa mfano aweze kuwafundisha wengine ili waweze kufanikiwa kiuzalishaji kama yeye.Anasema nidhamu katika kufuata ushauri wa wataalamu wa kilimo na matumizi sahihi wa pembejeo za kilimo yamemsadia kumletea mafanikio aliyonayo.

Pia aliongeza kuwa pamoja na kulima korosho analima mahindi ambayo msimu huu amevuna gunia 100, njugu mawe gunia 20 , Muhogo tani 10 . Mkulima huyo ana ng'ombe wa maziwa 20, kuku wa nyama na mayai na mashine ya kusaga na kukoboa nafaka. Akimalizia maelezo yake Mkulima huyo amesema kuwa ukulima wa korosho ni sehemu ya ulinzi wa mazingira kwa kuwa Korosho ni mti unaohitaji mvua kiasi, na una uwezo wa kuwa kijani bila kupoteza ukijani wake kwa mwaka mzima.

Aidha, korosho hupunguzwa matawi na kuweza kutumika kama chanzo cha nishati ya kuni , matunda yake kama kinywaji au tunda unaloweza kulila na zaidi hutumika kutengeneza Pombe ambayo ni chanzo kingine cha mapato.

Korosho ina uwezo wa kuwa na kilimo mchanganyiko yaani unaweza kulima

Baadhi ya wafanyakazi katika kiwanda cha Micronics System Limited wakifanya uchambuzi wa korosho.

mazao mengine kama mikunde ambayo inarutubisha ardhi. Pamoja na kupata faida ya kuzalisha chakula kingine kwenye eneo hilo hilo.

Naye Mkulima wa kijiji cha Mcholo Bibi Halima Malolo amesema "Nina jumla ya hekari 4 ambazo nalima korosho na nimeweza kuzalisha tani 4 ambazo zimenipatia kipato cha kuweza kujikimu mimi na familia yangu".

Bi Malolo ameongeza kuwa uzalishaji kwa sasa ni mzuri unalipa ila changamoto iliyopo kwa kinamama wazalishaji na wabanguaji wadogowadogo ni kupata mashine za kukaushia korosho ili nao waweze kubangua na kukausha na kupata masoko ya ndani na nje ya nchi ambao wanapenda zaidi korosho nyeupe tofauti na za kahawia ambazo zinapendwa na Watanzania.

Aidha, tunaomba Serikali ya Awamu ya Tano ifikirie kutupatia mashine za kukaushia korosho.

Bi. Malolo ameishukuru Serikali kwa kumpatia mafunzo mbalimbali ya ukulima wa korosho pamoja na kuhudhuria maonesho ya NaneNane katika Mikoa ya Lindi, Dodoma, Mbeya, Arusha na maonesho ya Sabasaba Jijini Dar-es-salaam.

"Hii imenisaidia kuwa na uelewa mpana wa utafutaji wa Masoko na kuwa na mtandao mzuri wa kuuza korosho ninazozalisha". alimaliza Bi Malolo.

Akiongea na mmoja wa wafanyakazi wa kiwanda cha Micronix System LTD Bi Rotha Minja ameishukuru Serikali ya Awamu ya Tano kwa kufufua viwanda vya kubangua korosho kwani vimesaidia kwa kiasi kikubwa kuboresha hali za maisha, ikiwa ni pamoja na kumudu kuhudumia watoto na kuwasomesha wakiwa nadhifu, wameshiba na wenye afya.

Pamoja na hayo kiwanda kimetupatia bima ya afya ya mwaka mmoja kila mfanyakazi na familia yake, sisi

Mwekezaji wa Kiwanda cha kubangua korosho cha Micronics System LTD kilichopo Newala, Mkoani Mtwara Bw. Sunil Kawath akitoa maelezo kwa Maafisa wa Serikali waliotembelea kiwanda hicho hivi karibuni..

tunachangia makato ya mfuko wa hifadhi ya jamii wa NSSF kwa asilimia 10 na muajiri anakatwa asilimia 10.

"Isitoshe tunapata chakula cha mchana hapa kazini kwa kweli kama Tanzania ya viwanda iko hivi tunakila sababu ya kumuombea Mhe Rais wetu Mungu ampe maisha marefu azidi kuboresha hali zetu za maisha". Alieleza Bi Ritha.

Msimu wa kilimo wa mwaka 2015/2016 korosho ghafi ilikuwa ikiuzwa Shilingi 1000 hadi 1200 kwa kilo. Msimu uliofuata wa 2016/2017 korosho ghafi ilipanda bei hadi kufikia 2000 mpaka 3600 kwa kilo na msimu wa mwaka 2017/2018 bei ilipanda zaidi na kufikia Tshs 4000 kwa kilo.

Mafanikio haya ya zao la korosho hayakuja kwa bahati tu ni pamoja na juhudi za makusudi kabisa Serikali kupambana na wale wote waliokuwa na nia ovu ya kuliharibia zao la korosho. Pamoja kurekebisha baadhi ya mambo yaliyokuwa yanakwamiza zao hili ikiwa ni pamoja na upatikanaji wa pembejeo kwa wakati, kupokea kilo za mkulima mmoja mmoja kwa usahihi katika vyama vya ushirika vya msingi na kuweka kumbukumbu. Pia, uwasilishaji wa kilo hizo za korosho katika chama kikuu cha ushirika – MUCOS na kufanya mnada wa wazi ambao unampatia kila mkulima fedha yake taslim bila kukopwa.

Mfanyakazi wa Kiwanda cha kubangua korosho cha Micronics System LTD sehemu ya Mtwara, Mjini Bi. Rotha Minja akieleza namna wanavyofungasha Korosho iliyobanguliwa kwa ajili ya kusafirishwa nje ya Nchi.

NUKUU YA LEO

KUTOKA KAMUSI KUU YA KISWAHILI

KIJUNGUJIKO

A. ***Kiasi au kiwango kidogo cha malipo/fedha ambacho hakitoshelezi mahitaji kwa mwezi***

B. ***Chakula kidogo kinachopikwa na kuishia kuliwa jikoni.***

NCHI YETU KATIKA PICHA

Wataalamu wa ujenzi kutoka kampuni ya Yapi Merkezi wakiwa wamekamilisha kuweka daraja la kwanza eneo la Shaurimoyo, Dar es Salaam ikiwa ni miongoni mwa vipande 100 vya madaraja ya juu yatakayoiwezesha treni ya SGR kupita juu kwa kilometa 2.8 kukwepa muingiliano na magari katikati ya jiji la Dar es Salaam.

Jengo la Hospitali ya kisasa ya Mkoa wa Simiyu ambalo ujenzi wake utakamilika mwaka huu ikiwa ni miongoni mwa majengo ambayo yametumia kiasi cha Bil.1. 7 zilizotolewa na Serikali.

Msemaji Mkuu wa Serikali, Dkt. Hassan Abbasi akitazama nguo ambazo zimetengenezwa hapa nchini kupitia uwekezaji chini ya Mamlaka ya Kusimamia Kanda Maalum za Kiuchumi (EPZA) alipotembelea Maonesho ya Kimataifa ya Dar es Salaam hivi karibuni

Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji Mhe. Charles Mwijage akipata maelezo kutoka kwa Mtafiti Msaidizi wa CAMARTEC, Mhandisi. Noela Byabachwezi kuhusu zana za kilimo zinazotengenezwa na kampuni hiyo, alipotembelea Maonesho ya Kimataifa ya Dar es Salaam hivi karibuni

NCHI YETU KATIKA HISTORIA

Hayati Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere (katikati) akishiriki katika uzinduzi wa mbio za magari za East Afrika Safari Machi 30, 1972

Mabalozi wa Tanzania waliopo nchi za nje wakitembelea kijiji cha Ujamaa cha Kawawa Mkoani Mtwara ili kuona makazi mapya ya wananchi, Machi 17, 1969

Hayati Waziri Mkuu, Edward Moringe Sokoine akiongea na wakazi wa kijiji cha Ujamaa na Ulinzi cha Mazinguri Wilaya ya Masasi ambapo aliwaomba kuwa makini na hila za mabepari, Septemba 13, 1977



Wanakijiji cha Ujamaa cha Lulanzi, Iringa wakiwa kiwandani wakitengeneza Makoroboi na Ndoo

MV Mwanza Mkombozi wa Wananchi Kigongo – Busisi

Kivuko cha MV. Mwanza kikiwa ndani ya Ziwa Victoria, kivuko hicho kitaanza kutoa huduma ya usafiri na usafirishaji wa abiria na mizigo kati ya Kigongo Misungwi na Busisi Sengerema mkoani Mwanza.

Na. Mwandishi Wetu -MAELEZO

Kasi ya uimarishaji wa miundombinu ya usafiri na usafirishaji kwa njia ya maji na utekelezaji wa ahadi vinazidi kuonekana baada ya kukamilika kwa ujenzi wa kivuko kipya cha MV Mwanza, Juni Mwaka huu.

Ujio wa kivuko hiki ambacho Watanzania wameshuhudia kwa mara ya kwanza kikiingia majini kwa majaribio ni utekelezaji wa ahadi aliyoitoa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt John Pombe Magufuli kwa wananchi wa Mkoa wa Mwanza na vitongoji vyake wakati wa kampeni za kugombea kiti cha urais mwaka 2015.

Ziwa Victoria ni miongoni mwa maziwa yenye visiwa vingi vidogo vidogo ambapo wakazi wake kulazimika kuvuka upande mmoja kwenda upande wa pili kwa njia ya maji hivyo kuwepo umuhimu wa kuongezeka kwa vyombo vya usafiri majini ili kurahisisha maendeleo ya wananchi na ukuaji wa uchumi.

Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, John Mongela amepongeza Wakala wa Ufundi na Umeme (TAMESA) kwa usimamizi mzuri wa mradi wa ujenzi wa Kivuko cha MV Mwanza uliofanywa na kampuni ya kizalendo ya Songoro Marine Boatyard Ltd ya Jijini Mwanza na kueleza kuwa kukamilika kwa ujenzi wa kivuko hicho kutaondoa changamoto za usafiri na usafirishaji si tu kwa wakazi wa eneo la Busisi, bali hata kwa abiria wa nchi za maziwa makuu wanaofanya shughuli zao kupitia Ziwa Victoria.

Kwa mujibu wa Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Songoro Marine Transport Bwana Salehe Songoro, kivuko cha MV Mwanza kitaanza kufanya kazi ya kuvusha abiria kutoka Kigongo wilayani Misungwi kwenda Busisi - Sengerema kuanzia Julai mwaka huu hatua itakayoondoa adha iliyokuwepo katika eneo hilo la Busisi.

Kivuko cha MV Mwanza kilianza kuundwa Mwezi Juni, 2016 na Kampuni ya Songoro Marine Transport ya Jijini Mwanza kwa gharama ya shilingi bilioni 8.9, uwezo wa kubeba abiria zaidi ya 800, magari 36 na uwezo wa kwenda kasi ukilinganisha na vivuko vingine vitatu vilivyopo, MV Sengerema, MV Sabasaba na MV Misungwi.

Machi, mwaka 2017 aliyekuwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano Prof, Makame Mbarawa alipokuwa

Kivuko cha MV. Mwanza kikiwa juu ya mifuko ya hewa kabla ya kushushwa majini ndani ya Ziwa Victoria katika ufukwe wa karakana ya kampuni hiyo Ilemela hivi karibuni Mkoani Mwanza.

akikagua maendeleo ya ujenzi wa kivuko cha MV Kazi ambacho pia kimetengenezwa jijini Dar es salam na Kampuni ya Songoro Marine Transport na kukabidhiwa Machi 12, 2017 alitoa rai TAMESA kushiriki kikamilifu shughuli za matengenezo ya vivuko ili kupata ujuzi wa ufungaji wa mifumo kutoka Kampuni zinazotengeneza vivuko vya serikali.

"Hakikisheni mnapata ujuzi kama walionao hawa, hatutaki kutumia fedha za Serikali kwa ajili ya kukarabati au kutengeneza vivuko wakati ninyi TAMESA mpo", alisema Prof. Mbarawa.

Hatua ya Kampuni ya Songoro Marine Transport kushiriki katika ujenzi wa vivuko mbalimbali hapa nchini inatoa taswira nzuri kwa umma na kuonesha namna ambavyo Serikali ipo tayari kutoa nafasi kwa wazawa kushiriki katika ujenzi wa maendeleo ya nchi yao.

Kuongezeka kwa kivuko cha MV Mwanza ambacho kimetengenezwa kisasa zaidi huku kikiwa na uwezo wa kwenda kwa kasi kuliko vivuko vingine vilivyopo eneo la Busisi, kitaongeza kwa abiria wa mikoa ya Mwanza kuelekea Geita, Kigoma, Kagera na hata nchi jirani za Rwanda na Burundi.

Tanzania ya viwanda yenye uchumi wa kati kufikia mwaka 2025 inawezekana.

Tuunge mkono juhudi zinazofanywa na Serikali kuimarisha huduma za usafiri na usafirishaji kwa njia ya maji kwa kutumia miundombinu hii iliyoboreshwa ili kuleta maendeleo yetu na taifa.

Wananchi wakishuhudia kivuko cha MV. Mwanza kikishushwa majini baada ya ujenzi wake kukamilika ambapo kitaanza kutoa huduma ya kusafirisha mizigo kati ya Kigongo Misungwi na Busisi Sengerema mkoani Mwanza.

Maafisa kutoka DAWASA, wakiangalia sehemu ya mabwawa ikiwa ni harakati za kuweka mfumo wa maji safi katika kambi ya wajenzi, eneo la kuzalisha umeme wa Stiegler's kwa sasa 'The Rufiji Hydropower Project (RHPP) wilayani Rufiji mkoani Pwani.

Wanaobeza Mradi wa Stieglers Gorge Wapuuzwe

Na. Mwandishi Wetu - MAELEZO

Kumekuwa na mwendelezo wa mjadala katika mitandao ya kijamii kuwa mradi wa umeme kwa kutumia maji unaotarajiwa kuanza kujengwa katika kipindi hiki cha Serikali ya Awamu ya Tano hauna tija wala hauna manufaa kwa watanzania.

Hoja hii mufilisi ambayo kwa kiasi kikubwa imebebwa na wanasiasa uchwara ambao wamekosa hoja, inalenga kuwaaminisha wananchi kuwa kila kinachofanyika na Serikali ya Rais Magufuli hakilengi kuinua maisha yao kama adhma ya Serikali kabla ya uchaguzi ilivyokusudia.

Kufilisika kwa hoja kwa wanasiasa hasa tunapoelekea katika uchumi wa kati unaoshabihishwa na ukuaji wa viwanda hakuwezi kufanikiwa kama hakuna umeme wa kutosha na wa uhakika.

Mosi, wanaobeza juhudi hizi hawajui kwamba mataifa makubwa duniani pia yanategemea uzalishaji wa nishati ya umeme kwa kutumia maji.

Pili uzalishaji wa umeme kwa kutumia maji ndio pekee unaozifanya nchi za Scandinavia kuzalisha umeme mwingi na wa uhakika ambao wanaweza pia kuwauzia nchi majirani tena kwa bei nafuu kabisa, japo wana vyanzo vingine vya umeme kama umemejua, upepo na kadhalika.

Kwa taarifa ya wanaobeza mradi wa umeme wa stieglers Gorge kwa sasa 'The Rufiji Hydropower Project (RHPP), ni kwamba gharama za matengenezo ya mtambo wa kuzalisha umeme kwa kutumia gesi kwa mwaka,mfano kituo kimoja tu cha Kinyerezi I ni Shilingi bilioni 15, wakati gharama za matengenezo ya kituo cha kuzalisha umeme kwa njia ya maji cha kidatu ni Shilingi bilioni 2.5 tu kwa mwaka, kwa hali ya kawaida na kwa mtanzania hata asiye na elimu ni kipi rahisi kati ya hivyo viwili?.

Kwa mujibu wa wataalam wa masuala ya umeme uzalishaji wa umeme kwa kutumia gesi unahitaji fedha nyingi za matengenezo kwenye mitambo yake kwa kuwa mitambo yake huchemka sana kwa zaidi ya digrii 2000 hivyo kuhitaji matengenezo ya mara kwa mara lakini

Sehemu ya Bwawa ambalo DAWASA wamejenga kwa ajili ya kuweka mfumo wa maji safi katika kambi ya wajenzi eneo la kuzalisha umeme wa Stiegler's kwa sasa 'The Rufiji Hydropower Project (RHPP).

pia kuhitaji kubadilisha vifaa kila baada ya muda flani, hii ni tofauti na matumizi ya maji ambapo mtambo wa kuzalisha umeme huchemka kwa digrii 50 tu hivyo kutohitaji matengenezo ya mara kwa mara na yenye gharama kubwa.

Kwa ufafanuzi huo ni wazi kuwa umuhimu wa mradi wa Rufiji Hydropower Project ni mkubwa tunapoelekea Tanzania ya viwanda na hii ni kutokana na ukweli kwamba vyanzo vingine vya umeme sio vya uhakika sana kutokana na mifumo yake ya uzalishaji

wa umeme. Mfano ukitegemea umeme wa upepo siku kusipokuwepo na upepo ina maana hakutakuwa na umeme. Pia ukitegemea umeme wa jua siku kama hakuna jua ama mvua imenyesha mfululizo kwa wiki nzima inamaana hakutakuwa na umeme.

Ni vyema wale wanaobeza uanzishwaji wa mradi huu kwa kudandia hoja bila kufanya utafiti wa kina basi waelewe kuwa mradi huu ni muhimu sana kwa taifa hasa tunapoelekea katika Tanzania ya viwanda.

Pia mradi huu haukuibuka tu katika awamu hii ya uongozi wa Rais Magufuli, kwa mara ya kwanza mradi uliibuliwa mwaka 1980 na wataalam waliofanya utafiti na upembuzi yakinifu wakati ule walieleza kwenye taarifa zao kwamba mradi huo hauna athari zozote za kimazingira.

Mradi haukuanza katika miaka ile kwa kukosekana kwa fedha lakini kwa sasa fedha za kutekeleza mradi huo zipo na nia ya dhati ipo hivyo uungwe mkono ili tusonge mbele.

> wanaobeza juhudi hizi hawajui kwamba mataifa makubwa duniani pia yanategemea uzalishaji wa nishati ya umeme kwa kutumia maji.

Kipimo cha kupimia kina cha maji (water gauge) katika sehemu ya Mto Rufiji uliopo katika wilaya ya Rufiji mkoani Pwani, utakapojengwa mradi wa Stieglers Gorge wa kuzalisha umeme kwa kutumia nguvu za maji (The Rufiji Hydropower Project -RHPP) ambao utazalisha umeme wa Megawati 2100 .

Serikali Yasisitiza Matumizi ya Nishati Mbadala Kuhifadhi Mazingira



Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan akimkabidhi Bw. Leonard Kushoka (wa pili kulia) mfano wa hundi yenye thamani ya shilingi milioni 300 mara baada ya kuibuka mshindi wa shindano la teknolojia ya nishati mbadala wa mkaa mwaka 2018, wengine pichani ni Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira Mhe. January Makamba (mwenye suti ya bluu) na Mwenyekiti Mkazi wa Kampuni ya Shell Bw. Axel Knospe.

Na. Fatma Salum - MAELEZO

Serikali imewasisitiza wananchi na Taasisi za Serikali kuacha matumizi ya mkaa na badala yake watumie nishati mbadala ili kuepuka changamoto za uharibifu mkubwa wa mazingira unaoendelea nchini nzima kutokana na matumizi ya mkaa.

Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Kassim Majaliwa aliyasema hayo hivi karibuni wakati akizindua Wiki ya Mazingira katika Viwanja vya Mnazi Mmoja, Jijini Dar es Salaam, ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya siku ya Mazingira duniani iliyofanyika Juni 5 mwaka huu.

Mheshimiwa Majaliwa aliziagiza Wizara na Taasisi zote za Serikali ambazo zinatumia mkaa kama nishati kuacha mara moja na badala yake zitumie nishati mbadala ili kupunguza uharibifu mkubwa wa mazingira unaoendelea hapa nchini.

"Baadhi ya Taasisi za Serikali kama Magereza, Jeshi, shule na hospitali zinaongoza kwa matumizi makubwa ya mkaa na kuni kwenye kupikia, hivyo naziagiza taasisi hizo kuacha kutumia kuni na mkaa ili kupunguza uharibifu wa misitu yetu," alisema Mheshimiwa Majaliwa.

Kwa upande wake Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), January Makamba, alisema kuwa maadhimisho hayo kitaifa yalifanyika Jijini Dar es Salaam kwa lengo la kuwapa fursa wananchi wa Jiji la Dar es Salaam kuelimishwa na kuhamasishwa kupambana na changamoto za uharibifu wa mazingira unaolikumba jiji hilo, ikiwemo mafuriko, uchafuzi wa mazingira utokanao na plastiki, kubomoka kwa kuta za fukwe za Bahari ya Hindi pamoja na utumiaji wa kiasi kikubwa cha nishati ya mkaa.

Waziri Mkuu, Mhe. Kassim Majaliwa akipata maelezo kutoka kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Space Engineering Limited, Bw. Philip Mtui kuhusu mkaa uliotengenezwa kutokana na takataka na kufungashwa kwenye kiroba tayari kwa kuuzwa wakati alipotembelea banda la Kampuni hiyo kabla ya kuzindua Wiki ya Mazingira kwenye viwanja vya Mnazi Mmoja jijini Dar es salaam, Mei 31, 2018. Katikati ni Mkuu wa mkoa wa Pwani Mhandisi, Evarest Ndikilo.

Waziri Makamba alieleza kuwa matumizi makubwa ya mkaa hayapo tu katika Jiji la Dar es Salaam bali pia katika maeneo mengine ya nchi, hivyo kutokana na matumizi makubwa ya nishati hiyo, kaulimbiu ya maadhimisho ya mwaka huu ni; "Mkaa Gharama; Tumia Nishati Mbadala".

"Nasisitiza kuwa sote tuna jukumu la kuanza kubadilika kutoka kwenye matumizi ya mkaa na kuanza kutumia nishati mbadala wa mkaa.

Tukumbuke kwamba suala la kuhifadhi mazingira ni jukumu letu sote na tunapaswa kulitekeleza kwa vitendo,"alisema Makamba.

Alibainisha kuwa takwimu zinaonyesha kwamba mpaka mwaka 2017 kiasi cha hekta 46,942 za misitu huharibiwa kila mwaka kwa ajili ya kupata mkaa ambapo matumizi makubwa yako katika miji mikubwa ikiwemo Dar es Salaam, ambako wastani wa tani 500,000 za mkaa hutumiwa kila mwaka.

Waziri Makamba alieleza kuwa uharibifu wa misitu unasababisha kuwepo kwa changamoto nyingine za mazingira kama vile ukame, majangwa, uharibifu wa ardhi, upotevu wa mimea asilia, upotevu wa viumbe hai mbalimbali, upungufu wa upatikanaji wa maji na upungufu wa uzalishaji kwenye kilimo.

Aidha Waziri Makamba alitoa wito kwa mikoa mingine nchini kushiriki kikamilifu katika utunzaji wa mazingira kwa kuhamasishana, kelimishana masuala yanayohusu hifadhi ya mazingira.

Tarehe 5 Juni, 2018 watanzania waliungana na nchi nyingine duniani kuadhimisha Siku ya Mazingira Duniani.

Maadhimisho ya Siku ya Mazingira yaliamuliwa mwaka 1972, katika mji wa Stockholm nchini Sweden, kwenye mkutano wa kwanza wa Umoja wa Mataifa uliohusu Mazingira.

Mwaka huu maadhimisho hayo kimataifa yalifanyika nchini India katika mji wa New Delhi. Kauli mbiu ya maadhimisho hayo kimataifa ni "Beat Plastic Pollution" ambayo inahimiza jamii kuepuka uchafuzi wa mazingira utokanao na plastiki.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais, (Muungano na Mazingira), Mhe. January Makamba akipata maelezo juu ya hatua mbalimbali za uzalishaji wa nishati mbadala kutoka kwa Bw. Leonard Kushoka.

Tanzania Yatangaza Fursa Zake za Uwekezaji Ughaibuni

Sehemu ya washiriki wa kongamano la Biashara na Uwekezaji kati ya Ujerumani na Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki wakifuatilia mawasilisho ya mada ya juu ya hali ya uchumi kwa nchi za Afrika Mashariki

Na. Immaculate Makilika na Latifa Kigoda-MAELEZO

Tanzania ni kati ya nchi chache ulimwenguni ambazo zimejaliwa kuwa na raslimali za kila aina kama vile madini ya aina mbalimbali yakiwemo Tanzanite ambayo hupatikana Tanzania pekee, nishati kama vile gesi asilia, vivutio vya utalii ikiwemo Mlima Kilimanjaro ambao ni mrefu kuliko yote barani Afrika, pamoja na mbuga za wanyama za Serengeti, Ngorongoro, Manyara, Mikumi na nyinginezo.

Ili kuhakikisha utajiri huo unatumika vizuri kwa manufaa ya taifa, mapema mwezi huu, Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikianio wa Afrika Mashariki Balozi Dkt.Augustine Mahiga, Balozi wa Tanzania nchini Sweden Dkt. Wilbroad Silaa, Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC) Bw. Geoffrey Mwambe pamoja na Mkurugenzi Mtendaji Shirika la Utangazaji la Taifa Dkt. Ayoub Rioba wameshiriki katika mkutano wa fursa za uwekezaji Tanzania uliofanyika huko Stockholm nchini Sweden.

Lengo la mkutano huo likiwa ni kuwataka wanadiaspora na wageni kuja kuwekeza nchini, ambapo pia walipata fursa ya kuwasilisha changamoto wanazokabiliana nazo katika mazingira ya uwekezaji hapa nchini.

Waziri Mahiga amewataka watanzania waishio nje kuja kuchangamkia fursa za uwekezaji, " fursa zilizopo Tanzania hazihitaji kusubiri mabadiliko ya Katiba Mpya ili kuzipata, muda ni sasa wa kuingia katika ubia wa kibiashara, kuwekeza katika sekta zenye fursa ikiwemo kilimo na uwekezaji wa viwanda unaoendelea kwa sasa" alieleza Waziri Mahiga.

Aidha, katika mkutano huo Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Uwekezaji Tanzania Geoffrey Mwambe, aliwasilisha mada iliyoeleza kuhusu fursa za uwekezaji na mahitaji ya vipaumbele vya Taifa, huku akisisitiza Tanzania ni tajiri kuliko nchi nyingine duniani, hasa katika maeneo ya raslimali ikiwemo ardhi yenye rutuba, lakini pia inashika nafasi ya saba kwa vivutio barani Afrika, sambamba na kuwa na mazingira yanayovutia.

Aidha, katika kuendeleza mkakati huo wa serikali wa kutangaza fursa za uwekezaji nchini ili kuvutia wawekezaji kutoka maeneo mbalimbali duniani kuja kuwekeza, Mkurugenzi Mtendaji huyo wa TIC, aliendelea na kufanya mikutano hiyo katika nchi za Uholanzi na Ujerumani ambapo amesaini makubaliano ya ushirikiano na Taasisi ya Biashara za Kimataifa ya Uholanzi (DCIB) pamoja na kufanya mkutano na baadhi ya wafanyabiashara wa taifa hilo wenye nia ya kuja kuwekeza katika sekta mbalimbali ikiwa ni pamoja na mafuta, gesi, kilimo, afya, usafirishaji, viwanda, fedha, mazingira, nishati na mawasiliano.

Makubaliano hayo yatakayodumu kwa kipindi cha miaka mitano yana malengo ya kubadilishana taarifa za fursa na mazingira ya uwekezaji, kuratibu ujio wa wafanyabiashara wa Uholanzi kuja kuwekeza pamoja na kufanya biashara nchini, pia Watanzania kwenda Uholanzi. Halikadhalika, kukijengea uwezo Kituo cha Uwekezaji kufanya kazi zake za kutafiti, kuhamasisha na kufanikisha uwekezaji na kukuza sekta binafsi ya Tanzania hususan

wawekezaji wa ndani na wajasiriamali kupitia mafunzo mbalimbali.

Katika hatua nyingine, Mwambe aliwahakikishia wawekezaji wa kutoka nchini Ujerumani na duniani kwa ujumla kuwa Tanzania ni nchi yenye fursa nyingi na mahali salama kwa uwekezaji ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki na Afrika, hivyo wawekezaji wenye mitaji na teknolojia wanakaribishwa kuja kuwekeza kwenye sekta mbalimbali ambazo kwa sasa ni kipaumbele cha Taifa hususan eneo la viwanda, kilimo, madini, mifugo, uvuvi, miundombinu, uzalishaji na usambazaji umeme na miundombinu kwa ujumla.

Naye mwakilishi wa Benki ya Stanbic kwa Kanda ya Afrika Mashariki Bw. Jibran Qureishi ameeleza kuwa kwa sasa Tanzania inafanya vizuri katika masuala ya kiuchumi ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki na Afrika kwa ujumla.

Matokeo hayo chanya ni kutokana na uongozi mahiri wa Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli aliyeanzisha vita ya kupambana na rushwa na kupunguza urasimu kwa lengo la kuweka mazingira wezeshi ya uwekezaji.

Bw. Qureishi alisema kuwa "Tanzania ina nafasi kubwa ya kuendelea kufanya vizuri zaidi katika nyanja ya uchumi na kwa miaka ya hivi karibuni baada ya kukamilika kwa miradi mikubwa ya maendeleo inayotekelezwa na Serikali kwa kutumia rasilimali za ndani na sio mikopo kama ilivyokuwa imezoeleka". Huku akitaja baadhi ya miradi hiyo kuwa ni ya kuzalisha umeme wa Stiegler's Gorge, ujenzi wa reli ya kisasa pamoja na upanuzi wa bandari. Hakuna shaka kuwa, mtaji mkubwa na jambo adhimu linavutia kuja kuwekeza nchini Tanzania ni uwepo wa amani na matumizi ya lugha ya Kiswahili ni kati ya nyenzo muhimu zitakazotumika kulifikisha Taifa hili katika uchumi wa kati ifikapo 2025 na kulipatia maendeleo zaidi. Hivyo ni vyema watanzania wakaendelea kudumisha amani iliyopo sambamba na kukuza matumizi ya lugha hii adhimu ambayo ni ya pili kwa kuwa na wazungumzaji wengi barani Afrika, huku ikiwa lugha ya 10 kwa kuwa na wazungumzaji wengi zaidi duniani ambapo inakadiriwa kuzungumzwa na watu takribani milioni 200 duniani kote.

Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC), Bw. Geoffrey Mwambe, (kulia waliokaa) na Mwenyekiti wa Taasisi ya Biashara za Kimataifa ya Uholanzi (DCIB), Bw. Hans Biesheuvel (Kushoto waliokaa) wakisaini makubaliano ya ushirikiano.



Mfumo wa TEHAMA Waboresha Huduma za Jamii



Afisa TEHAMA, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Bw. Robert Dudu akiwaelekeza Maafisa TEHAMA kutoka Halmashauri za Mikoa ya Dodoma, Singida, Arusha, Shinyanga, Kigoma na Manyara namna mfumo mpya wa malipo (epicor 10.2) unavyofanya kazi, hivi karibuni Jijini Dodoma.

Na. Frank Mvungi - MAELEZO

Tanzania imepata mafanikio makubwa katika kutoa huduma za jamii kwa kutumia mifumo ya TEHAMA iliyokokatikaMamlakazaSerikalizaMitaa

Hatua ya kuimarishwa kwa mifumo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) katika mamlaka hizo ni chachu katika utoaji wa huduma bora za jamii kama vile afya, elimu na hata ukusanyaji wa mapato ambapo kwa sasa wigo wake umepanuka zaidi kuliko ilivyokuwa awali kabla ya kuwepo kwa mifumo huo.

Rais wa Serikali ya Awamu ya Tano Dkt. John Pombe Magufuli mara nyingi amekuwa akipambanua kuwa Serikali yake imejikita katika kuwahudumia wananchi wanyonge hasa katika maeneo ya vijijini. Ili huduma hiyo itolewe kwa ufanisi watendaji wote wanalazimika kutumia mifumo ya TEHAMA kwa ajili ya mawasiliano na ukusanyaji wa mapato.

Ni dhahiri kwamba mabilioni ya shilingi yanayotumika kila mwezi kugharamia elimu bure na pia katika kununua madawa kwa ajili ya hospitali, vituo vya afya na Zahanati, yanatokana na matumizi mazuri ya mifumo madhubuti ya TEHAMA. Huduma hizo ni ishara ya wazi katika kusimamia rasilimali zilizopo kwa maslahi ya wananchi wanyonge

Hapana shaka kuwa kuimarishwa kwa mifumo kama ule wa kubainisha mahitaji ya watumishi katika vituo vya kutolea huduma za afya (WISN) na ule unaotumika katika kuwapangia vituo vya kazi yaani POA,kutasaidia kuondoa malalamiko ya kukosekana kwa uwiano wa watumishi kati ya kituo kiomoja na kingine katika halmashauri zetu hapa nchini.

Akizungumza jijini Mbeya wakati wa mafunzo ya matumizi ya mifumo ya WISN na POA kwa Watumishi wa Sekta ya Afya, Utawala na Serikali za Mitaa, Mkuu wa Timu ya Mifumo ya Rasilimali Watu kutoka Mradi wa Kuimarisha Mifumo ya Sekta za Umma (PS3), Dkt. Josephine Kimaro, amesema kuwa lengo la mifumo hiyo ni kusaidia kuboresha huduma zinazotolewa kwa wananchi kupitia vituo vya kutolea huduma za afya.

Akifafanua, Dkt. Kimaro amesema kuwa Ofisi ya Rais- TAMISEMIkwa kushirikiana na mradi wa PS3 wanafanya kazi yakuhakikisha watumishi katika sekta ya afya wanapelekwa kwenye maeneo yenye uhitaji, ili kuongeza ubora wa huduma zinazotolewa kwa kuzingatia dhamira ya Serikali ya Awamu ya Tano inayoongozwa na Rais Dkt. John Pombe Magufuli.

Kwa upande wake Katibu Tawala Msaidizi Utawala na Rasilimali watu mkoa wa Mbeya, Bw. Marko Masaya, amesema kuwa mifumo hiyo imekuja wakati muafaka na itasaidia kurahisisha uandaaji wa mipango ya ajira kwa watumishi wapya kulingana na mahitaji, na kubainisha maeneo watakapopelekwa baada ya kuajiriwa.

"Mifumo hii inaongea, hali itakayosadia kubainisha uwiano wa majukumu kati ya mtumishi mmoja na mwingine katika vituo vya kutolea huduma, hivyo tutabaini watumishi wanatekeleza majukumu mengi zaidi kuliko inavyotakiwa ili tuweze kuongeza watumishi wengine katika eneo hilo," alisisitiza Masaya Akieleza zaidi, amesema kuwa moja ya hatua zitakazochukuliwa ili kuhakikisha kuwa mifumo hiyo inaleta matokeo chanya,mkoa huo utaongeza

usimamizi kwa watoa huduma katika vituo vya kutolea huduma ili takwimu zinazokusanywa kupitia mifumo hiyo ziwe halisi na hivyo kusaidia katika kuimarisha huduma kwa wananchi.

Dhamira yangu si kuchambua mifumo hii bali kuonesha kinaga ubaga jinsi Serikali ya awamu ya Tano ilivyojikita katika kuwahudumia wananchi wanyonge kwa kuweka mifumo imara na inayoendana na mahitaji na changamoto zinazowakabili wananchi katika maeneo ya kutolea huduma hasa za afya.

Kuwepo kwa uwiano wa watumishi kutokana na uwepo wa mifumo ya WISN na POA katika vituo vya Afya si tu kutaboresha huduma zinazotolewa bali ni chachu kwa Taifa letu kukuza uchumi na ustawi wa watu wake, lengo au azma ya kuwa na wananchi wenye afya bora liliasisiwa na Serikali ya Awamu ya kwanza chini ya Mwalimu Julius Kamnbarage Nyerere ambaye alijipambanua katika kupigana na maadui maradhi, ujinga na umasikini. Kujengwa kwa mifumo hii kumeenda sambamba na kuendeshwa kwa mafunzo kwa watumiaji wa mifumo wa sekta zote husika ikiwemo wahasibu, wagavi, waweka hazina, maafisa Tehama, waganga wakuu wa wilaya, watunza kumbukumbu za afya na makatibu wa afya.

Mafunzo hayo yanaendeshwa na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) kwa ufadhili wa Serikali ya Marekani kupitia Shirika la Maendeleo ya Kimataifa la Marekani (USAID) na kutekelezwa kupitia mradi wa uimarishaji wa mifumo ya sekta za umma (PS3). Mradi huu ni wa miaka mitano na unatekelezwa katika mikoa 13 ya Tanzania bara.

Akizungumza katika mahojiano maalum jijini Mbeya mkurugenzi wa TEHAMA kutoka Ofisi ya Rais - TAMISEMI Bw. Erick Kitali alibainisha kuwa,moja ya mambo makubwa yanayopaswa kuzingatiwa na kusisitizwa ni swala la uzalendo kwa watumiaji wa mifumo hii katika kuwahudumia wananchi.

Amesema Serikali imeonesha dhamira ya dhati ya kushirikiana na wadau kama mradi wa uimarishaji mifumo katika sekta za umma (PS3) kuimarisha mifumo mingine kama Epicor 10.2 iliyoboreshwa hali itakayosaidia halmashauri na mikoa kutekeleza dhana ya uwazi na uwajibikaji kwa wananchi.

Nae Mkuu wa Timu ya Mifumo ya TEHAMA kutoka PS3, Bw. Desderi Wangaa alieleza "Faida za mifumo hii ni pamoja na kuongeza uwazi na uwajibikaji katika mamlaka za serikali za mitaa ambapo wananchi sasa wanaweza kushiriki kikamilifu katika kusimamia rasilimali fedha zinazotolewa kwa ajili ya miradi ya maendeleo".

Kupitia mifumo kama PlanRep Serikali inatumia gharama ndogo katika kuandaa mipango na bajeti na utoaji wa ripoti katika halmashuri zote hapa nchini. Kazi zote zinazofanyika katika halmashuri na mikoa hutumia mfumo huu katika kuwasilisha bajeti na mipango Ofisi ya Rais TAMISEMI.

PONGEZI KWA RAIS, DKT. JOHN POMBE MAGUFULI

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt John Magufuli akisisitiza jambo kwa wadau wa sekta ya kilimo wakati wa uzinduzi wa Program ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo Awamu ya Pili (ASDP II) hivi karibuni jijini Dar es Salaam.

ASDP II Mkombozi Sekta ya Kilimo na Ufugaji

Na. Judith Mhina - MAELEZO

Hivi karibuni Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt John Pombe Joseph Magufuli alizindua Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo Awamu ya Pili (ASDP II) iliyoanza mwaka wa fedha 2017-2018 na itamalizika mwaka 2027- 2028.

Akizindua Programu hiyo, Rais Magufuli alisema kuwa, Programu hiyo ikifanya vema katika matumizi ya rasilimali maji, kujenga miundombinu na matumizi endelevu ya tekinolojia ya umwagiliaji, itawanufaisha wakulima na kuvutia wengi kuingia katika uzalishaji na kuongeza kasi ya uanzishwaji wa viwanda vitakavyotoa ajira hasa kundi la vijana.

"Tanzania imebahatika kuwa na vyanzo vingi vya maji kama maziwa, mito, mabwawa, na ardhi nzuri yenye rutuba. Hivyo tukijikita katika matumizi sahihi ya rasilimali maji na tekinolojia ya umwagiliaji tutazalisha kwa tija mazao ya chakula na biashara, malisho ya mifugo na samaki". Alieleza Rais Magufuli.

Alisema Uwepo wa Programu ya ASDP II ni kielelezo tosha kuwa Tanzania imeazimia kuzalisha kwa wingi kwa kuwa na watu zaidi ya milioni 50, ikilinganishwa na milioni 10 iliyokuwepo mara baada ya uhuru. Ambapo asilimia 70 ya idadi ya watu hivi sasa huishi kwa kutegemea kilimo cha mazao, ufugaji na uvuvi.

Alikielezea kilimo kama uti wa mgongo wa Taifa letu na kinachangia ukuaji wa uchumi kwa takriban asilimia 3.7 na kwamba Programu hiyo imelenga kutumia ipasavyo rasilimali maji na kujikita katika ujenzi wa miundombinu na matumizi ya teknolojia ya umwagiliaji ambayo itazalisha kwa tija mazao mbalimbali, pia programu itakuja na mbinu za hifadhi maji yatokanayo na mvua kwa ajili ya uzalishaji.

Kulingana na takwimu alizozitoa Kaimu Mkurugenzi wa Tume ya Taifa ya Umwagiliaji Mhandisi, Dkt. Eliakimu Chitutu, Tanzania kwa sasa ina ufanisi wa matumizi ya maji ulioongezeka kutoka asilimia 30 hadi asilimia 60 kwa kila msimu mmoja.

Aidha mpaka sasa kuna miradi 2,947 ya umwagiliaji nchi nzima". Hata hivyo, Rais Magufuli alieleza kutoridhishwa na kiwango hicho cha umwagiliaji na kuhimiza uanzishwaji na uendelezwaji wa kilimo cha mazao,

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt John Magufuli akionesha kitabu cha Program ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo Awamu ya Pili (ASDP II) kwa wadau wa sekta ya kilimo (hawapo pichani) mara baada ya kuzindua program hiyo hivi karibuni jijini Dar es Salaam.

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt John Magufuli akimkabidhi Rais Mstaafu wa Serikali ya awamu ya pili, Dkt. Ali Hassan Mwinyi, nakala ya programu ya kuendeleza kilimo awamu ya pili (ASDP II) mara baada ya uzinduzi wa program hiyo hivi karibuni jijini Dar es Salaam.

malisho ya mifugo na ufugaji wa samaki. Teknolojia hii ya umwagiliaji itafanikisha kuzalisha kwa tija na kupelekea kupata masoko ya ndani na kuhimili soko la nje lenye mahitaji makubwa wakati wote.

Uzalishaji wa aina hii utaifanya nchi kuwa na uhakika wa usalama wa chakula na kuzalisha kwa ubora unaotakiwa kitaifa na kimataifa. Aidha, viwanda vitaongezeka kwa kuwa malighafi za mazao zinapatikana, wakulima watapata malipo mazuri na kuwavutia vijana kuingia katika sekta ya kilimo na kupata ajira viwandani.

Alisisitiza kuwa teknolojia ya umwagiliaji ni muhimu kwa kuwa nchi itaepuka uzalishaji wa msimu wa mvua tu, ambao hauna nafasi katika soko la kimataifa. Pia, ASDP II imebuni na kutafuta mbinu zaidi zitakazoweza kukabiliana na majanga mbalimbali kama vile mafuriko, maporomoko ya udongo, ukame, magonjwa na dhoruba nyingine za kimazingira ili kuhimili na kuweza kuzalisha hata nyakati hizo ngumu. Akifafanua maeneo yaliyoainishwa kuwa yanafaa kwa umwagiliaji Chitutu amesema "kuna Jumla ya hekta milioni 294 kwa ajili ya kuendeleza umwagiliaji endelevu. Hadi kufikia Februari 2017 hekta zaidi ya 400,000 sawa na asilimia 1.6 la eneo lote linalofaa kwa umwagiliaji lilifikiwa".

Akionyesha mafanikio ya tekinolojia ya umwagiliaji Chitutu alisema kilimo cha Umwagiliaji kimechangia ongezeko la mpunga kutoka tani mbili, mpaka kufikia tani 5. Mahindi uzalishaji kutoka tani 3.7 mpaka kufikia tani tano kwa hekta moja.

Uzalishaji wa vitunguu umeongezeka kutoka tani 13 hadi tani 26 kwa hekta. Uzalishaji wa nyanya umeongezeka kutoka tani tano hadi tani 18 kwa hekta.

Kwa sasa eneo la uzalishaji la mazao ya umwagiliaji ni hekta 450,000 ambapo ASDP II imekusudia kufikia 600,000 mwaka 2028, na ifikapo 2030 lengo ni Kuongeza eneo la umwagiliaji mpaka kufikia hekta milioni moja.

Programu ya ASDP I ilianza mwaka wa fedha 2006/2007 na kukamilika mwaka 2012/2013, Kwa kujenga jumla ya miradi 241 ya umwagiliaji litekelezwa kwa kulima mazao ya mpunga, miwa, zabibu, kilimo cha mpunga mseto na ufugaji wa samaki, n.k Kati ya miradi hiyo, kuna ambayo ipo kwenye hali nzuri na mingine inahitaji ukarabati. Naye Afisa Mawasiliano wa Programu ya ASDP II Bi Happy Mlaki amesema kuwa programu itatekelezwa katika mikoa na wilaya zote za Tanzania Bara ambapo inakusudia kuwafikia wakulima wengi zaidi kulingana na miradi yenye mahitaji katika maeneo yao.

Wito wa Rais Magufuli kwa wale wote watakaohusika katika utekelezaji wa Programu hii, ni kuzingatia thamani ya fedha kwa kila kazi itakayofanyika. Pia kuhakikisha shughuli za kiutawala haziwi na matumizi makubwa ya fedha ikilinganishwa na makusudio matatu ya awali yaliyoainishwa katika Programu hiyo.

Akielezea mchango wa uzalishaji wa chakula, Waziri wa Kilimo, Dkt.Charles Tizeba amethibitisha kuwa Tanzania inakusudia kuwa ghala kuu la chakula barani Afrika kwa kuwa kwa miaka miwili mfululizo imeweza kuzalisha kwa asilimia 120 msimu wa mwaka 2016 na asilimia 123 msimu wa mwaka 2017, pamoja na soko la uhakika la Afrika takriban watu milioni 300 kwa sasa.

"Tukiwa na matumizi ya rasilimali maji, kujenga miundombinu na matumizi endelevu ya tekinolojia ya umwagiliaji, itasaidia kuwanufaisha wakulima na kuwavutia kuingia katika uzalishaji na kuongeza kasi ya uanzishwaji wa viwanda vitakavyotoa ajira hasa kundi la vijana.

Rais Dkt. Magufuli

LIMEANDALIWA NA

Idara ya Habari-MAELEZO
S.L.P 25
Dodoma-Tanzania
Simu : (+255) 22 -2122771
Baruapepe:maelezo@habari.go.tz
Tovuti: www.maelezo.go.tz
Blogu: blog.maelezo.go.tz

@TZMsemajiMkuu
Msemaji Mkuu wa Serikali
MaelezoTv